Mahojiano na watumizi wa huduma wa kike

Tarehe :	Jina la mwezeshaji:
Mtaa :	Jina la anayechukua matini:
Kaunti ndogo :	Kitengo cha kushiriki: watumizi wa huduma wa kike
Kaunti :	Kundi la umri (weka mviringo): 15-18; 19-24; 25-49
Nambari ya washiriki: #wenye wako kwa ndoa:	#wajawazito: #watoto wadogo:

Matini ya mwezeshaji:

- Kabla ya kuanza, Mwezeshaji ahakikishe fomu zote za wale watakaoshiriki zimewekwa sahii.
- Kundi likiwa tayari ,kabla ya mahojiano kuanza, mwezeshaji lazima aambie kikundi : Jina langu ni _____ na ninafanya kazi na mradi wa Afya Halisi .Ahsante kwa muda wako wa kuzungumza na sisi leo. Nataka kuchukua muda kuongea na wewe leo kuhusu mliyoyapitia na huduma za afya . Mwenzangu, _____ ako hapa kunisaidia kuchukua matini . Kushiriki kwako mazungumzo ya leo ni kwa hiari. Unaweza kujiondoa wakati wowote .Hutapoteza manufaa yoyote ikiwa hutashiriki. Vile vile hutapata manufaa ya ziada ikiwa utashiriki. Chochote tutazungumza hapa leo ni siri. Hakuna chochote utasema kitahusishwa na jina lako. Mazungumzo yasizidi masaa mawili. Kabla tuanze, una maswali yoyote?
- Jibu maswali yote, alafu uliza, Unaweza kuendelea?
- Mruhusu yeyote ambaye hangependa kuendelea, alafu anza mazungumzo.

I. Uliyoyapitia na huduma za malezi ya uja uzito

1. Wakati ulipokua mjamzito ya mwisho (ama kwa ujauzito wa sasa), ulienda ziara za malezi ya ujauzito mara ngapi? Mbona uliamua kuzuru mara nyingi hivyo? (*Dokeza: ni nini au ni nani alishawishi maamuzi yako?*)
2. Mume wako/mwenzako alichukuliaje ziara zako za malezi ya ujauzito? Alikusaidia kufika? Ikiwa ndio,vipi?
3. Mume wako/mwenzako alikuja na wewe? Mbona au mbona hakuja? Ulimtaka afike na wewe? Mbona au mbona hukutaka?
4. Ni muhudumu yupi uliona katika ziara ya ANC ? alikua wa kike au wa kiume?
5. Muhudumu alikushughulikia vipi? (*dokeza: wakisema"vizuri" ama "vibaya" au jibu lolote fupi , uliza, "ni nini walifanya hadi ukahisi kwamba umeshughulikiwa vizuri?")*Ulijihisi vizuri na umeheshimiwa? Mbona au mbona hukujihisi hivyo?
6. Unafikiria ungehudumiwa vyema ikiwa mume wako/mwenzako angekuja na wewe? Mbona au mbona hufikirii hivyo? (*Ikiwa wanawake wengi walienda ANC na wenzao, uliza, "unafikiri ungehudumiwa tofauti ungekuwa pekeyako? Mbona au mbona hufikirii hivyo?")*

II. Uliyoyapitia leba na huduma za kujifungua

1. Ulijifungulia mtoto wako wa mwisho wapi? (kwa wale ambao ni wajawazito kwa mara yao ya kwanza, uliza, “unapanga kujifungulia wapi?”) ni nini kilipelekea uamuzi huu?(Dokeza: ni nini au ni nani alishawishi uamuzi huu?)
2. Kwa wale waliojifungulia kituoni, nani alikuja na wewe? Nani aliamua kuwa mtu huyo aje na wewe? Kuna mwingine yeyote ungependa aje na wewe? (Dokeza: kama waume/wenzao hawajatajwa hapa, uliza, “vipi kuhusu mwenzako?”)
3. Muhudumu wako alikushughulikia vipi? (Dokeza: wakisema “vizuri” ama“vibaya” au jibu lolote fupi , uliza, “ni nini walifanya hadi ukahisi kwamba umeshughulikiwa vizuri?”)Ulijihisi vizuri na umeheshimiwa? Mbona au mbona hukujihisi hivyo?
4. Unafikiria ungehudumiwa vyema ikiwa mume wako/mwenzako angekuja na wewe? Mbona au mbona hufikirii hivyo? (Ikiwa wanawake wengi walienda na wenzao, uliza, “unafikiri ungehudumiwa tofauti ungekuwa pekeyako? Mbona au mbona hufikirii hivyo?”)
5. Kuzingatia uliyoyapitia, utamwambia nini rafiki anayejaribu kuamua ikiwa atajifungulia kituoni au la?

III. Uliyoyapitia na huduma za FP

1. Kama mojawapo ya huduma zako za ANC, kujifungua, au PNC , ulipewa ushauri kuhusu upangaji uzazi? Kama ndio, uliambiwa nini?
2. Mipango yako ni ipi kuhusu kutumia au kutotumia upangaji uzazi siku za usoni? Sababu za uamuzi huu ni zipi?
3. Unajadili upangaji uzazi na nani? Nani hufanya uamuzi wa mwisho kuhusu kutumia au kutotumia mbinu, na aina ya mbinu?

IV. Uliyoyapitia na lishe na WASH

1. Nani hufanya haya kwa familia yako:
   - Kutafuta maji ya matumizi nyumbani
   - Kufyeka eneo karibu na nyumba
   - Mifugo wanaoishi kwa boma
2. Ni changamoto zipi kwa watoto/wasichana/wanawake kutumia choo na kupata vishodo?
3. Je walezi uwaweka mahali tofauti pa kucheza watoto wavulana wachanga na wasichana wachanga ama wakati walezi wanafanya kazi za nyumbani? Kama ndio, eleza tofauti hizi.
4. Nani uamua aina na kiwango cha chakula kipewacho mtoto wa kiume? Mtoto wa kike? *(Dokeza, majukumu ya baba? Nyanya(mama mkwe)?*)
5. Mbona inakua vigumu kuwapa watoto aina tofauti ya vyakula (kama vile nyama, maziwa, mboga za majani, matunda)?
6. Mwanamume hufanya nini kumsaidia mkewe kunyonyesha au kulisha watoto wadogo? (*dokeza majukumu ya mwanamume kwa kulisha watoto wachanga/watoto wadogo*)

Matini ya mwezeshaji:

- Baada ya swali la mwisho kuulizwa, ambia (wa)mshiriki: Tumefika mwisho wa mahojiano yetu. Kabla tufunge, una maswali yoyote ya mwisho kwangu?
- Jibu maswali yaliyobaki, alafu washukuru washiriki kwa muda wao.
- Waeleze washiriki ikiwa kuna chochote wanaitaji kufanya ili kupata malipo yao ya nauli

Mahojiano na wasiotumia huduma wa kike

Tarehe :	Jina la mwezeshaji:
Mtaa :	Jina la anayechukua matini:
Kaunti ndogo:	Kitengo cha kushiriki: Wasiotumia huduma wa kike
Kaunti :	Kundi la miaka (weka mviringo): 15-18; 19-24; 25-49
Nambari ya washiriki: #wenye wako kwa ndoa:	#wajawazito: #watoto wachanga:

Matini ya mwezeshaji:

- Kabla ya kuanza, Mwezeshaji ahakikishe fomu zote za wale watakaoshiriki zimewekwa sahii.
- Kundi likiwa tayari ,kabla ya mahojiano kuanza, mwezeshaji lazima aambie kikundi : Jina langu ni _____ na ninafanya kazi na mradi wa Afya Halisi .Ahsante kwa muda wako wa kuzungumza na sisi leo. Nataka kuchukua muda kuongea na wewe leo kuhusu mliyoyapitia na huduma za afya . Mwenzangu, _____ ako hapa kunisaidia kuchukua matini . Kushiriki kwako mazungumzo ya leo ni kwa hiari. Unaweza kujiondoa wakati wowote .Hutapoteza manufaa yoyote ikiwa hutashiriki. Vile vile hutapata manufaa ya ziada ikiwa utashiriki. Chochote tutazungumza hapa leo ni siri. Hakuna chochote utasema kitahusishwa na jina lako. Mazungumzo yasizidi masaa mawili. Kabla tuanze, una maswali yoyote?
- Jibu maswali yote, alafu uliza, Unaweza kuendelea?
- Mruhusu yeyote ambaye hangependa kuendelea, alafu anza mahojiano.

I. Uliyoyapitia na huduma za malezi ya uja uzito

1. Wakati ulipokua mjamzito ya mwisho (ama kwa ujauzito wa sasa), ulienda ziara za malezi ya ujauzito mara ngapi? Mbona uliamua kuzuru mara nyingi hivyo? (*Dokeza: ni nini au ni nani alishawishi maamuzi yako?*)
2. Mume wako/mwenzako alichukuliaje ziara zako za malezi ya ujauzito? Alikusaidia kufika? Ikiwa ndio,vipi?
3. Mume wako/mwenzako alikuja na wewe? Mbona au mbona hakuja? Ulimtaka afike na wewe? Mbona au mbona hukutaka?
    - Matini ya mwezeshaji: kama hakuna yeyote kwa kikundi alienda ANC , uliza, “ungelipenda mume wako aende na wewe? Mbona au mbona hungelitaka?”
4. Ni muhudumu yupi uliona katika ziara ya ANC ? alikua wa kike au wa kiume?
    - Matini ya mwezeshaji: Ruka ikiwa hakuna yeyote aliyefika ziara za ANC .
5. Muhudumu alikushughulikia vipi? (dokeza: wakisema“vizuri” ama “vibaya” au jibu lolote fupi , uliza, “ni nini walifanya hadi ukahisi kwamba umeshughulikiwa vizuri?”)Ulijihisi vizuri na umeheshimiwa? Mbona au mbona hukujihisi hivyo?
    - Matini ya mwezeshaji: ikiwa hakuna yeyote aliyefika ziara za ANC , uliza, “unadhani wahudumu wanawashughulikia wanawake vipi katika hizi ziara zao za ANC ? Ikiwa watatoa jibu la neon moja , kama, “vizuri” au “vibaya” dokeza: Ni nini wanafanya kinachokufanya useme hivi?”
6. Unafikiria wanawake wanahudumiwa tofauti ikiwa wako na wenzao? Mbona au mbona hufikirii hivyo? (Ikiwa wanawake wengi walienda ANC na wenzao, uliza, “unafikiri wanawake wangehudumiwa tofauti wangekuwa pekeyao ANC? Mbona au mbona hufikirii hivyo?”)

II. Uliyoyapitia leba na huduma za kujifungua

1. Ulijifungulia mtoto wako wa mwisho wapi? (kwa wale ambao ni wajawazito kwa mara yao ya kwanza, uliza, “unapanga kujifungulia wapi?”) ni nini kilipelekea uamuzi huu?(Dokeza: ni nini au ni nani alishawishi uamuzi huu?)
2. Kwa wale waliojifungulia kituoni, nani alikuja na wewe? Nani aliamua kuwa mtu huyo aje na wewe? Kuna mwingine yeyote ungependa aje na wewe? (Dokeza: kama waume/wenzao hawajatajwa hapa, uliza, “vipi kuhusu mwenzako?”)
3. Kwa wale waliojifungulia kituoni, nani alikua na wewe ukijifungua? Nani aliamua kuwa mtu huyo awe na wewe? Kuna mwingine yeyote ungependa awe na wewe? (Dokeza: kama waume/wenzao hawajatajwa hapa, uliza, “vipi kuhusu mwenzako?”)
4. Muhudumu wako alikushughulikia vipi? (Dokeza: wakisema “vizuri” ama“vibaya” au jibu lolote fupi , uliza, “ni nini walifanya hadi ukahisi kwamba umeshughulikiwa vizuri?”)Ulijihisi vizuri na umeheshimiwa? Mbona au mbona hukujihisi hivyo
   - Matini ya mwezeshaji: kama hakuna yeyote alijifungulia kituoni, uliza,“Unafikiri wahudumu huwashughulikia vipi wanawake ambao huja kujifungua? Wakitoa jibu la neon moja , kama, “vizuri” au “vibaya” Dokeza: wanafanya nini ili useme haya?”
5. Unafikiri wanawake watahudumiwa tofauti wakiwa na wenzao? Mbona au mbona hufikirii hivyo?
6. Kuzingatia uliyoyapitia ukijifungua, utamwambia nini rafiki anayejaribu kuamua ikiwa atajifungulia kituoni au la?

III. Uliyoyapitia na huduma za FP

7. Umewahi pokea ushauri kuhusu upangaji uzazi? Kama ndio, lini? Uliambiwa nini?
8. Mipango yako ni ipi kuhusu kutumia au kutotumia upangaji uzazi siku za usoni? Sababu za uamuzi huu ni zipi?
9. Unajadili upangaji uzazi na nani? Nani hufanya uamuzi wa mwisho kuhusu kutumia au kutotumia mbinu, na aina ya mbinu?

IV. Uliyoyapitia na lishe na WASH

1. Nani hufanya haya kwa familia yako:
   - Kutafuta maji ya matumizi nyumbani
   - Kufyeka eneo karibu na nyumba
   - Mifugo wanaoishi kwa boma
2. Ni changamoto zipi kwa watoto/wasichana/wanawake kutumia choo na kupata vishodo?
3. Je walezi uwaweka mahali tofauti pa kucheza watoto wavulana wachanga na wasichana wachanga ama wakati walezi wanafanya kazi za nyumbani? Kama ndio, eleza tofauti hizi.
4. Nani uamua aina na kiwango cha chakula kipewacho mtoto wa kiume? Mtoto wa kike? *(Dokeza, majukumu ya baba? nyanya?*)
5. Mbona inakua vigumu kuwapa watoto aina tofauti ya vyakula (kama vile nyama, maziwa, mboga za majani, matunda)?

6. Mwanamume hufanya nini kumsaidia mkewe kunyonyesha au kulisha watoto wadogo? (*dokeza majukumu ya mwanamume kwa kulisha watoto wachanga/watoto wadogo*)

Matini ya mwezeshaji:

- Baada ya swali la mwisho kuulizwa, ambia (wa)mshiriki: Tumefika mwisho wa mahojiano yetu. Kabla tufunge, una maswali yoyote ya mwisho kwangu?
- Jibu maswali yaliyobaki, alafu washukuru washiriki kwa muda wao.
- Waeleze washiriki ikiwa kuna chochote wanaitaji kufanya ili kupata malipo yao ya nauli